**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**640** **HISABATI**

**Muda: Saa 3** **Mwaka: 2020**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16).**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali wawili katika kila sehemu **B** na **C.**
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na kila sehemu **B** na **C** ina alama **thelathini (30).**
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhiswa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

2 103021 100228



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (alama 40)**

Jibu maswali **yote**

1. Kokotoa $3\frac{1}{2} - 1\frac{3}{4} \div 2\frac{2}{3} + 4\frac{1}{4} \times 1\frac{2}{5}$.

2. Tafuta eneo la uso wa tufe lenye nusu kipenyo cha sentimita 7.

3. Tafuta Kigawe Kidogo cha Shirika (KDS) cha:

   (a) $10a$ na $8a$.

   (b) $3y$ na $6x$.

4. Tafuta riba kwa muda wa miaka 5 ikiwa kianzio kisichobadilika ni shilingi 2,000,000 na kima ni asilimia 6 kwa mwaka.

5. Tafuta namba mbili zinazofuatana ambazo jumla yake ni 4,325.

6. Tafuta muungano wa seti P = {1, 2, 3, 4, 5} na Q = {4, 5, 6, 7}.

7. Fumbua mlinganyo $5(2a - 3) - 3(2a + 1) = 0$.

8. Taja faida nne za upimaji katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Hisabati.

9. Badili:

   (a) kilomita 4.6 kuwa sentimita.

   (b) sentimita 15 kuwa milimita.

10. Iwapo watu 20 hulima shamba kwa siku 8, je watu 16 watalima shamba hilo kwa siku ngapi?



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU B (alama 30)


Jibu maswali **mawili (2)**

11. (a) Iwapo A = {0,1,2,3, 4,5,6} na B = {1, 2,3, 4,8,9} chora mchoro wa Venn kuonesha:

(i) $A \cup B$ (ii) $A \cap B$

(b) Katika darasa lenye wanafunzi 35, wanafunzi 17 hujifunza Hisabati na 11 hujifunza Hisabati na ICT. Iwapo wanafunzi 7 hawajifunzi Hisabati wala ICT, ni wanafunzi wangapi hujifunza ICT? Tumia mchoro wa Venn katika kujibu swali hili.

12. Kijiji cha Songambele kilipata faida ya Shilingi 414,000 kwa kuuza mazao ya nafaka kama ilivyooneshwa kwenye grafu kwa duara lifuatalo:




(a) Je, kijiji kilipata kiasi gani cha faida kwenye mauzo ya kila zao?

(b) Je, ni zao lipi lilipata faida kubwa ukilinganisha na mazao mengine?

13. (a) Taja aina tatu za namba nzima na toa mfano kwa kila moja.

(b) Kokotoa $(-2)^3$



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU C (alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)**

14. (a) Eleza jinsi utakavyowafundisha wanafunzi wa Darasa la Kwanza dhana ya $\frac{1}{4}$ kwa mara ya kwanza.

(b) Onesha utakavyomfundisha mwanafunzi wa Darasa la Saba dhana ya kuwa $+3 + -7 = -4$ kwa kutumia mstari wa namba.

15. Eleza utakavyomfundisha mwanafunzi kutafuta jumla ya $\frac{7}{8}$ na $\frac{1}{2}$ kwa kutumia kielelezo cha mstatili.

16. (a) Eleza kwa kutoa hoja nne jinsi utakavyowafundisha wanafunzi wa Darasa la Tano kuchora pembe yenye nyuzi 60 kwa kutumia Bikari.

(b) Onesha hatua utakazotumia kumfundisha mwanafunzi jinsi ya kuchora pembe yenye nyuzi 90 kwa kutumia Bikari na Rula pekee.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org